Teacher.co.ke

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

## KISWAHILI FASIHI 102/3

## KIDATO CHA NNE MUHULA WA PILI 2024

***USHAIRI***

i) Shairi huru (1 x 1 = alama 1)

ii) Vina vinabadilikabadilka.

Idadi ya mizani katika kila mishororo ni tofauti.

Idadi ya vipande si sawa katika kila msororo.

Shairi halina kibwagizo. (zozote 3x1 = alama 3)

iii)Uhuru / idhini ya mshairi

Kuboronga sarufi mf. Nje na ndani ya nyumba watazunguka – watazunguka nje na ndani ya nyumba n.k.

Inkisari mf. Kaziyo – kazi yako. (2 x 2 = alama 4)

iv)Uhaishaji – Jingi jasho likuoshe.

Tanakuzi – Nje na ndani ya nyumba usiku mchana uwasake.

Taswira – Kifo cha mende … sharti miguu juu.

Ufyeke, upime na uweke nguzo, kisha paa uweke na ukandike. (alama 4x1=4)

v) Na uweke dawa nyingi hata nyumba.

Uihame na ukae nje siku nzima ukisubiri.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Ukirudi usiku, bado utakuta ni wazima.

Wamelala kwani mende ni vichwa vigumu.

Hawafi kwa urahisi. (zozote 4x1 = alama 4)

(vi) Ukijenga nyumba yako, hutakaa sana bila kuingiliwa na wageni.

Hata mende wataanza kutalii bila ruhusa na bila woga wakila ulichonacho wakuachie masalio.

Hata ukiweka dawa hawafi.

Mende wakifa ni sharti miguu iwe juu.

Haiwezekani mtu kuishi pweke kwenya nyumba. (zozote 2x1 = alama 2)

(vii) Kisha paa uweke na ukaandike

Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa (1 x 1 = alama 1)

(viii) Mende

Kifo cha mende

Mende nyumbani (alama 1 x 1 =1)

**Bembea ya Maisha**

2 a i). Maneno ya Yona kwa Sara. Wamo nyumbani. wanazungumzia suala la Neema kuwafaa wazazi wake wakati wa uhitaji. (4x1=alama 4)

ii) Mdokezo. mfano kama…

Tashbihi - kama tambara (2x1=alama2)

b. Anaingia nyumbani na kuulizia chakula-hili linazua mgogoro kati yake na Sara.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Anataka Neema awasaidie kwa sababu alimsomesha

Analewa na kupoteza kazi

Anashiriki vikao vya wazee

Anawatunza mifugo yake.

Anaacha pombe na kuanza kumsaidia Sara.

(Zozote 4x1=4)

c**) Mila na desturi/utamaduni**

i)Yona anaambia Sara kuwa fimbo ya mzee(majukumu) hurithiwa na mtoto wa kwanza (uk, 2).

ii) Dina anaambia Kiwa watu waliuliza na wanauliza nani atarithi ardhi ya Yona

iii)Yona anataka kujua sababu ya Sara kutomwandalia chochote(uk. 13)

iv)Sara anaambia Dina mila imewafanya wanaume kuwaachia wanawake kazi zote za nyumbani.

iv)Sara anaambia Dina watu wakijua mume anamsaidia mke jikoni watasema hadhi yake imeshushwa, kwa mizani ya jamii mwanamke atakuwa amejivua nguo (uk. 14).

vi)Neema anamwambia Bela kuwa wazee wake hawawezi kulala kwa mkwe wao (uk. 24).

vii)Wazazi wa Bunju walipokuwa hai hawakuwahi kuja kuishi kwake(uk.29).

viii)Bunju anaambia Neema kuwa hawezi akakaa na wazazi wa Neema kwake, ni laana.

ix)Sara anaambia Asna kuwa ikiwa Yona ataonekana akiteka maji kisimani kijiji kitasema kwamba amewasomesha watoto ambao wamemweka Sara jijini ili Yona ataabike; watamdharau(uk 45).

x)Luka anaambia Yona na Beni kuwa zamani ilikuwa ni desturi mavuno ya kwanza kuonjwa na wazee ili kutoa baraka(uk.58).

xi)Sara anaambia Neema binti za mama anayemzuia mumewe kufanya atakayo (anayemtilia mguu wa kausha) hawaolewi, huzeekea nyumbani (uk. 66).

xii)Sara anamwambia Neema utamaduni haumruhusu mwanamke kushindana na mwanamume.Kulingana na Sara,hekima si hekima itokapo kwa mwanamke.(uk 68)

xiii).wanawake ni wategemezi kwa waume zao. ( Zozote 10x1=10)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

5. Tofauti za ukale na usasa

a) i)Elimu ya mtoto wa kike hapo awali haikudhaminiwa lakini sasa inadhaminiwa .Tunaona Sara hakuweza kukamilisha masomo yake alifika darasa la saba lakini Neema amesoma na kuhitimu ana digrii mbili.

ii)Wanawake wa awali walitegemea mifuko ya waume zao lakini siku hizi wanajitegemea kifedha .Neema anategemea mshahara wake kufanya mambo kadha.

iii) Michezo ya watoto zamani haikugharimu chochote.Leo lazima ilipiwe kama Bunju anavyosema.

iv) Mavuno ya kwanza hapo zamani yalionjwa na wazee ili kutoa baraka siku hizi hali hii haizingatiwi.

v) Watoto wa zamani walilelewa vizuri katika utamaduni na lugha zao asili.Yona anasema kuwa wajukuu wake hata neno moja la lugha yao asili hawajui.

vi )Safari za zamani zilichosha kutokana na barabara bovu, siku hizi usafiri ni mwema kwa sababu barabara zimesakafiwa.

vii) Wanaume hawakuingia jikoni hapo awali sasa wanafanya hivyo tunaona Yona akitayarisha kiamsha kinywa.

Viii) Wanawake wa awali waliozwa pindi tu walipobaleghe lakini sasa wanasoma na kujiamulia wakati wao.

ix) Nyimbo za siku hizi si kama za zamani. Watoto wa siku hizi lazima warukaruke .Bela anapoeleza sababu ya Lemi kufika nyumbani akiwa amechelewa.

x) Zamani wazazi hawangeishi na watoto wao katika nyumba moja lakini sasa wapo wazazi wanaofanya hivyo.

xi) Wanawake wa zamani walidhamini kuwa wanene lakini wa siku hizi wanang’ang’ania kukonda-asemavyo Asna.

xii)Watoto wa kike zamani hawakuruhusiwa kwenda shuleni.Sasa wanakwenda.

xiii) Watoto wa zamani waliadhibiwa kwa kiboko shuleni lakini siku hizi huwezi kumnyoosha mtoto kwa kiboko.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

xiv) Watu wa zamani walikutana wakala na kunywa pamoja hukuna wakibadilishana mawazo lakini siku hizi hawazingatii haya.

xv)Watoto wa kike zamani hawakurithi kitu. Wa sasa wanarithi.

usasa (10x1=alama10)ukale (10x1=alama 10)jumla alama20

**Nguu za jadi**.

***Swali la nne***

4a) Mnenaji:Mrima

Mnenewa:Mangwasha

Mahali:nyumbani mwao.

Ni baada ya Mangwasha kumsaili mumewe Mrima uhusiano wake na Sangilu. (alama 4x1=4)

b.)Maudhui ya taasubi ya kiume. (alama 2x1=2)

c.)i.Vingozi wengi nchini matuo ni wanaume.

ii.Chifu Mshabaha anamwiita Mangwasha ofisini na kumkemea.

iii.Mrima anamtukana Mangwasha na kumtishia kuoa mke mwingine.

iv.Sagilu anajaribu njia zote kuhakikisha Mangwasha amekuwa mpenziwe.

v. Mtemi Lesulia anataka kumpa Nanzia talaka kwa kukosa kumpa mtoto.

vi.Mrima anadai tamaduni zinamkataza kutunzwa na kulelewa na mwanamke.

vii.Ngoswe anadai wanawake walimfuata mwanaume yeyote bora awe na pesa.

viii.Ngoswe anawabadilisha wanawake kila uchao.

ix.Mbungulu anamkubusha Mangwasha kuwa hafai kumfuata mumewe katika starehe zake.

x.Mrima anamwaambia Mangwasha kuwa hawezi kumzuia kuoa wanawake anaotaka.

xi.Mrima anamwaambia Mangwasha kazi ya mke ni kuzaa,kulea na kushughulikia mambo ya nyumbani.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

xii.Mwanaume anachukuliwa kama kichwa na mwanamke kama shingo.

xiii.Mke hawezi kumuuliza mumewe aendako au atokako.

Xiv.Mbungulu anashauri majaoni hapakuwa mahali pa wanawake.

xx.Wanaume ndio wanaopaswa kuhutubia jamii. **(alama14x1=14)**

***Swali la tano*.**

5.Tamaa ni hali ya kutaka sana kitu, matamanio ya kitu au jambo.

Ubinafsi hubainika pale mtu anapojipendelea yeye au kujifikiria yeye mwenyewe bila ya kuwajali wengine.

---

1.Mtemi Lesulia anajawa na tamaa ya uongozi. Anamteka nyara Lonare asiweze kuwa katika kinyang'anyiro cha uchaguzi mkuu anapohisi kwamba huenda akamshinda na kuwa mtemi.

2.Mtemi Lesulia akiwa na wakwasi wenzake kama vile Sagilu na Mbwashu wanahujumu pato la nchi kutokana na tamaa ya kujilimbikizia mali.

3.Ubinafsi wa Mtemi Lesulia unaonekana pale anapomiliki rasilimali za serikali hasa kupitia kwa unyakuzi unaoendelezwa na mkewe Nanzia.

4.Nanzia anaonyesha tamaa na ubinafsi pale anapojaribu kubinafsisha jumba la Skyline Mall ambalo ni mali ya serikali (uk. 147) na ardhi ya Matango kwa kushirikiana na mafisadi wenzake.

5.Sagilu anaendeleza maudhui ya tamaa na ubinafsi pale utashi wake wa pesa unampofanya kuhodhi bidhaa kama vile ngano ili kuiuza kwa bei ya juu .

6.Sagilu kutokana na tamaa anahatarisha maisha ya watoto nchini Matuo anapoagiza maziwa yenye sumu kutoka ughaibuni (uk. 17). Ubinafsi wake unamfanya kuwazuia wengine wasimpiku kibiashara.

7.Tamaa ya uongozi na mali inamwingizaSagilu katika urafiki na mtemi ili kutosheleza maslahi ya kibinafsi.

8.Ubinafsi pia unamfanya Sagilu kumtumia Mrima ili kujinufaisha kisiasa kutokana na tamaa ya uongozi.

9.Sagilu aliandamwa pia na tamaa za kimwili. Anawabadilisha wanawake hadi kuitwa dudumizi kutokana na kuvizia na kuwachukua wake wa wengine mfano Sihaba,kuzaa na mke wa mtemi Lesulia n.k

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

10.Mrima anaendeleza maudhui ya tamaa na ubinafsi pale ambapo tamaa ya pesa inamtosa katika tabia potovu. Anadanganywa na Sagilu huku akipewa pesa hadi kuitelekeza jamaa yake.

11.Ubinafsi wa kuyajali maslahi yake pekee unamfanya Mrima kukaidi masharti ya ndoa na uwajibikaji.

12.Ubinafsi wa Mafamba unamfanya kuhujumu sheria za nchi kwa kuutetea ufisadi serikalini.

13.Ubinafsi pia unamfanya kudanganya kuwa vyeti vya kumiliki ardhi vya wenyeji wa Matango vilikuwa ghushi. 14.Tamaa ya pesa inamfanya Sihaba kujiingiza katika biashara ya ulanguzi wa watoto wa kike (uk. 141-144).

15.Sihaba anatumiwa na Sagilu kuhujumu haki za Waketwa mbali na kutumiwa na Sagilu kuwaangamiza maadui zake kibiashara. (zozote kumi 10x2=20)

**Hadithi fupi.Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingineo.**

**Sabina.**

a)Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kukuza hadithi husika

*Mrejelewa ni Sabina*

i) Ametumiwa kuendeleza na kukuza ploti ya hadithi kutokana na mgogoro baina yake na familia ya Ombati..

ii) Ni kielelezo bora cha wanajamii wanaoenzi masomo na wanaojitolea sabili ili kupata ufanisi katika maisha yao ya halali.

iii)Mwandishi amemtumia kukashifu ukiukaji wa haki za watoto na kukandamizwa kwao.

iv)Ametumiwa kudhihirisha maudhui ya uwajibikaji, elimu na ukiukaji wa haki za watoto mayatima.

v)Ametumiwa kudhihirisha matatizo yanayopitiwa na watoto mayatima.

vi)Amechimuza sifa ya Ombati na Yunuke kama katili.

v)Ametumiwa kufanikisha methali baada ya dhiki faraja kwani anajipitia magumu mwanzoni lakini baadaye maisha yake yanaendelea.(uk. 94), na kwamba serikali ilitaka kujenga soko katika mtaa wa Matango.

vi)Anatambulisha wahusika kwa mfano Yanuke,Ombati n.k (alama6x1=6)

b) Aina za taswira katika kifungu.

i)Taswira sikivu mfano,...yalimwiingia Ombati maskioni.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

ii)Taswira oni mfano,…amevaa rinda kuukuu,walimzoa juujuu,kupigwa picha.

iii)Taswira mnuso mfano,…harufu ya samadi inamvuka.

iv)Taswira mguso mfano,…walimzoa juujuu. (alama 4x1=4)

(c)**Fafanua changamoto zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi**

•Wanajamii kumtenga Sabina wakidai familia yao iliandamwa na mikosi na nuksi.

•Sabina kudhulumiwa kwa kupigwa na Yunuke.

•Sabina kusongwa na mawazo kabla ya mtihani wa kitaifa.

•Sabina kupangiwa njama ya kuozwa mapema hata kabla ya kumaliza masomo yakc(wa darasa la nane )kuwadia.

•Sabina kufanyishwa kazi za sulubu na Yunuke.

•Nyaboke (mamake Sabina ) kupata ujazito akiwa umri mdogo.

•Sabina kulelewa na mzazi mmoja akiwa na umri mdogo.

•Nyaboke kulazimika kuacha shule baada ya kupata mimba.

•Babake Sabina kumkana Sabina baada ya kumkana Sabina mchana peupe.

•Sabina kuachwa yatima baada ya kifo cha mamake. Analazimika kuishi na babu na nyanya.

Sabina kudhulumiwa na Yunuke na kuambiwa kuwa juhudi zake katika masomo hazitafanikiwa. (alama 10x1=10)

7.**Swali la mzimu wa kipwerere**

a)Maneno ya msimulizi

Akimrejelea Bishoo

Yuko mzimuni wa Kipwerere

Msimulizi alikuwa amewafumania Bishoo na Salihina katika mzimu ambako alipata makasha ya tubako,robota ya bangi na mitungi ya chang'a.

(alama 4x1=4)

b i) Kubainisha mgogoro katika hadithi – mgogoro uliopo unaotokana na itikadi unaotumiwa na kina Salihina kuwalaghai wanakijiji.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

ii)Kuwatambulisha wahusika. Bishoo na Salihina

iii)Kuchimuza maudhui:ulaghai – Salihina anajifanya kuwa mdumishaji wa maadili ilhali yeye ndiye alikuwa akilangua dawa za kulevya.

iv)Kutambulisha sifa za wahusika: Bishoo anabainika kuwa mwongo kwa kuwa anamdanganya mumewe kuwa alikuwa akienda kumwona mtoto mgonjwa ilhali alikuwa anaenda kwa Salihina.

v)Kuibua dhamira ya mwandishi: Kuonyesha madhara ya ushirikina na itikadi: imani kuhusu Mzimu wa Kipwerere unawatia wanajamii hofu ilhali hakukuwa na mizimu au mashetani yoyote katika kichaka hicho.

vi.Kuendeleza ploti – kusuluhisha taharuki kuhusu kuwepo kwa mashetani katika mzimu kwa kuonyesha kuwa hakukuwa na shetani yeyote ila wajanja kama kina Salihina**.**

**Zozote 4 x 1 = 4**

c i) Tashbihi …meupe kama ya maiti, mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama.”

ii)Taswira oni… maguo yangu meupe (alama 2x1=2)

d i)Inaaminika kuwa yeyote aliyekiuka miiko kuhusu kutoingia katika mzimu angetolewa kama kafara kwa mizimu.

ii)Wanajamii wa eneo la Mzimu wa Kipwerere wanaamini kuwa Salihina angeweza kuwasiliana na mizimu. Hivyo, wanapotaka kuandaa sherehe kama vile jando wanamtuma Salihina kuzungumza na mizimu.

iii)Kuamini kwamba mwanamke na mwanamume waliozungumza walikuwa shetani na mkewe. Inadaiwa kuwa waliungumza wakati watoto wao walikuwa wamelala.

iv)Mashetani wanavuta sigara - Kuamini kwamba harufu ya sigara iliyotoka katika mzimu ilitokana na shetani aliyekuwa akivuta sigara.

v)Kuamini kwamba kulikuwa na wimbo uliokuwa kama ufunguo wa kuingia katika mzimu.

vi)Kuna itikadi kuhusu chanzo cha kichaka cha Mzimu wa Kipwerere – inaaminika kuwa kichaka hicho kilitokana na kaburi la mwanamke aliyeitwa Kipwerere.

vii)Wanajamii wa eneo la Kipwerere kutoruhusiwa kupita kichaka hicho saa sita mchana na usiku wote. Wanajamii hawakupewa sababu zenye mashiko za kuwanyima ruhusa ya kupitia kichaka hicho bali walitishiwa tu kuwa wangetolewa kama kafara kwa mzimu.

viii)Kuamini kwamba taa zilizowaka usiku katika Mzimu wa Kipwerere ziliwashwa na shetani wa mzimu ili kuwapa watoto wake chakula.

(alama 8x1=8)

**FASIHI SIMULIZI**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Swali la nane

a) i) Ulumbi ni uhodari wa kutumia lugha kwa ufundi wa kipekee. Ni utumiaji wa lugha kwa mvuto na ufasaha. ( alama 2x1=2)

ii) i)Hukuza uwezo wa kujieleza hadharani

ii)Hukuza ujuzi na ufasaha wa lugha

iii)Msingi wa kuteua viongozi

iv)Huhifadhi utamaduni wa jamii

v)Huburudisha

vi)Hukuza uzalendo

vii)Huweza kutumiwa kuwasilisha ujumbe muhimu

viii)Ni kitabulisho cha utabaka

Zozote 6 x 1= 6

iiii) a)Dhamira – lengo/nia inayokusudiana na hadithi

b)Maudhui- mambo yanayoelezwa katika hadithi k.m hekaya

c)Ploti – mtiririko wa utushi ama tukio katika hadithi.

d)Mandhari- mazingira ya wakati , hali au kimaeneo. Ya kuogofya, yenye misitu na majitu au mazimwi.

e)Wahusika- viumbe wa hadithi wa aina gani.

f)Usimulizi- hadithi inasimuliwa katika nafsi ya kwanza au ya tatu.

g)Muundo- miundo maalum ya kuanza na kufunga hadithi

h)Lugha- lugha ya moja kwa moja (sahili) na inayoweza kutumia tamathali za lugha.

(za kwanza sita 6 x 1= 6)

b) i) kuuliza maswali

ii) kujibu maswali

iii) kuwahusisha katika nyimbo

iv)kucheka pamoja

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

v)Kupiga makofi

vi)Kushangilia

vii)mdokezo

viii)Kuuliza maswali ya balagha ili kuibua hisia

ix)Mtuo wa kidrama. Zozote sita (6x1)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes